# Mitindo ya Lugha Inayomsawiri Mwanamke Kiongozi katika Tamthilia za *Pango* (2003) na *Kigogo* (2016)

Ogonda S. Sinzore, Deborah N. Amukowa na Beverlyne A. Ambuyo
Chuo Kikuu cha Maseno

**Ikisiri**

Tafiti nyingi zilizofanywa kumhusu mhusika mwanamke katika tamthilia za Kiswahili zilimsawiri mwanamke kwa ujumla bila kuangazia uongozi wake. Chache zilizoshughulikia mwanamke kiongozi zimefanya hivi bila kuangazia mitindo ya lugha inayochangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi. Mitindo ya lugha ni muhimu katika kuibua maudhui ya kazi ya fasihi. Makala hii ililenga kuchanganua mitindo ya lugha inayomsawiri mwanamke kiongozi katika tamthilia za *Pango* (Wamitila, 2003) na *Kigogo* (Kea, 2016). Zimelengwa tamthilia hizi kwa kuwa zimeandikwa baada ya mwaka 2000 ambapo hadhi ya mwanamke kiongozi imeendelea kuimarika na jamii kuonekana kukubali uongozi wa mwanamke. Tamthilia za *Pango* na *Kigogo* ziliteuliwa kupitia mbinu ya usampulishaji dhamirifu kwa kuwa zina wahusika wanawake ambao ni viongozi. Nadharia ya Udenguzi iliyoasisiwa na Derrida (1966) na kuelezwa na Ntarangwi (2004) iliteuliwa kwa ajili ya utafiti huu. Mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo (maudhui) ilitumiwa kukusanya data. Tamthilia teule zilisomwa na data kunukuliwa. Data ilipangwa kisha ikachanganuliwa kwa njia ya uhakiki wa yaliyomo. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Imebainika kupitia makala hii kuwa mitindo mbalimbali ya lugha imechangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia za *Pango* na *Kigogo*.

## 1.0 Utangulizi

Kimatumizi, neno ‘mwanamke’ huashiria mtu wa jinsi ya kike aliye na utu uzima au aliyekomaa na kufikia umri wa kuolewa ilhali mtu wa jinsi ya kike mwenye umri wa chini kuliko mwanamke au yule ambaye bado hajaolewa huitwa ‘msichana’ katika tamaduni nyingi ulimwenguni (Hora, 2014). Hata hivyo, neno mwanamke hutumiwa wakati mwingine kumtambulisha binadamu wa jinsi ya kike bila kujali umri. Mathalani, tunaposema haki za mwanamke tunaashiria haki ambazo mtu yeyote wa jinsi ya kike anazo au anastahili kuzipata pasipo kujali umri. Kwa minajili ya makala hii, dhana ya mwanamke imetumiwa kwa maana ya mtu yeyote wa jinsi ya kike bila kuzingatia umri.

Kwa mujibu wa TUKI (2014), kiongozi ni mtu anayesimamia na kuelekeza watu au kikundi cha watu, wafanyakazi au shughuli fulani. Kiongozi ni mkuu fulani. Kwa mujibu wa Mdee, Njogu na Shafi (2011), kiongozi ni mtu mwenye madaraka ya kuelekeza watu wengine. Vilevile, Kohlrieser (2006) anamfasili kiongozi kuwa ni mtu ambaye huwashawishi watu wengine kumfuata na kuwachochea watu kufikia malengo fulani. Kutokana na fasili hizi, ni bayana kwamba kiongozi ni mtu ambaye huelekeza na kuchochea watu kutekeleza shughuli fulani. Huenda kiongozi asiwe mkuu aliyechaguliwa kwa njia rasmi bali watu hutaka kumfuata kwa ajili ya mawazo mapya aliyonayo. Makala hii imezingatia mwanamke kiongozi kama mtu yeyote wa jinsi ya kike ambaye huwachochea na kuwaelekeza watu kutenda jambo fulani.

Mtindo ni jinsi ya kufanya kitu kwa kufuata taratibu fulani. Lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zinazotumiwa kwa mawasiliano miongoni mwa watu wa jamii fulani yenye utamaduni wake (Trudgil, 1974; TUKI, 2014). Wamitila (2003) anaeleza kuwa mitindo ya lugha ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Mitindo ya lugha ni muhimu katika kuibua maudhui ya kazi za fasihi (Mugambi, 1982; Murungi, 2013). Syambo na Mazrui (1992) wanasisitiza umuhimu wa lugha kwa kusema kwamba, lugha inahitaji kuwatofautisha wahusika kulingana na jinsi yao. Kulingana na Njogu na Chimerah (2007) mitindo ya lugha husaidia katika kuibua taswira ya wahusika katika kazi fulani ya kifasihi. Ipo haja ya kuhusisha mitindo ya lugha na suala la uongozi wa mwanamke kwani ni kupitia lugha ambapo taswira ya mwanamke kiongozi inaweza kubainika.

Momanyi (1998) anapendekeza kuwa wahakiki wa kisasa wawajibike katika kuhakiki usawiri wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili. Kulingana naye, hii itasaidia katika kubadilisha mielekeo ya watu kuhusu mwanamke kama kiambatisho au kitegemezi cha mwanamume. Utafiti huu umetekeleza pendekezo hili la Momanyi kwa kuchunguza namna mwanamke alivyosawiriwa kama kiongozi katika tamthilia za Kiswahili. King’ei (2002) anadai kuwa ni tafiti chache sana zilizozingatia kipengele cha matumizi ya lugha katika kubainisha masuala ya kiuana katika fasihi ya Kiswahili. Anashikilia kwamba, huo ni udhaifu mkubwa kwani lugha ndiyo njia muhimu zaidi inayotumika katika malezi na elimu, nyanja zinazochangia utu na mielekeo ya kijamii kuhusu uana kwa jumla. Makala hii imelenga kuziba pengo hili analolizungumzia King’ei kwa kuchunguza mitindo ya lugha inayochangia kujenga taswira ya kiongozi wa jinsi ya kike. Makala hii imegawanywa katika sehemu sita ambazo ni: utangulizi, nadharia iliyoongoza uchambuzi wa data, muhtasari kuhusu uongozi wa mwanamke katika tamthilia ya *Pango* (2003), muhtasari kuhusu uongozi wa mwanamke katika tamthilia ya *Kigogo* (2016), mitindo ya lugha inayojenga taswira ya mwanamke kiongozi na hitimisho.

## 2.0 Nadharia ya Udenguzi

Nadharia ya Udenguzi iliasisiwa na Jacques Derrida (1966). Nadharia hii hutupilia mbali dhana kuwa matini ya kifasihi huwa na lengo au maana moja (Miller, 1976). Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), nadharia hii hushikilia kuwa, kila msomaji binafsi huumba lengo na maana mpya na ya kibinafsi au ya kipekee katika matini. Ntarangwi anaendelea kueleza kuwa Nadharia ya Udenguzi huwa na mihimili mitatu mikuu: lugha, muktadha na mtazamo. Makala hii imeongozwa na mhimili wa lugha. Kulingana na Ntarangwi, nadharia hii hushikilia kuwa, lugha ni kipengele muhimu cha matini au usemi na kwamba lugha hubeba maana mbalimbali. Kwa mujibu wa Derrida (1973), lugha iliyotumiwa ndani ya matini huwa muhimu katika kuibua maana. Kulingana naye, maana hujiibua mbele ya mhakiki kama zulia linavyojikunjua mbele ya mtu anayelifungua kupitia kwa uchanganuzi wa lugha iliyotumiwa. Mawazo haya ndiyo yaliwafanya Njogu na Chimerah (2007) kusema kuwa kutokana na Nadharia ya Udenguzi hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Hivyo basi, wahakiki kwa misingi ya nadharia hii wanaweza kutoa fasiri tofautitofauti za jambo moja kwa kuchunguza lugha iliyotumiwa. Fasiri hizi kulingana na wawili hawa zinaweza kutofautiana au kufanana.

Kwa maoni ya Bakhtin (1981), lugha hubeba maana nyingi ndani ya matini. Lugha mbalimbali pamoja na matumizi mbalimbali ya lugha moja huugawa ulimwengu na kuupa maana mbalimbali. Kwa hivyo, hakuna maana moja ya neno au fungu la maneno katika kazi ya fasihi. Hadhira huibua maana mbalimbali kutokana na maneno aliyoyateua na kuyatumia mtunzi. Wahusika wa kazi ya fasihi wanapozungumza huleta maana mbalimbali zinazofasiriwa na wahusika wengine au wasomaji tofautitofauti. Kwa kutumia mhimili wa lugha katika Nadharia ya Udenguzi, tamthilia teule za Kiswahili zimesomwa huku lugha iliyotumiwa na wanawake viongozi pamoja na wahusika wengine ikichunguzwa ili kubaini inavyojenga taswira ya kiongozi wa jinsi ya kike katika tamthilia ya *Pango* na *Kigogo*.

## 3.0 Muhtasari kuhusu Uongozi wa Mwanamke katika Tamthilia ya *Pango*

Katango katika *Pango* (2003) anajitokeza kwa ujasiri kuwania uongozi. Kabla yake, hakuna mwanamke aliyekuwa amewahi kugombea wadhifa wa uongozi wa Pango. Kulingana naye, azma yake ya kuwania uongozi ni kuhakikisha kuwa kuna usawa Pangoni na kwamba asali ya Pango inamfaidi kila Mwanapango (uk. 28). Katango anaviziwa na Mtu I na II (waliotumwa na Ngwese ambaye ni mpinzani wa Katango) wakiwa njiani na Kibwana. Anatishwa, anafinywa, anabanwa na kutaka kubakwa ila hakati tamaa (uk. 31-33). Hatimaye, Katango anaibuka mshindi kama kiongozi wa Pango katika uwanja wa kampeni na kumpiku mpinzani wake, Ngwese. Ushindi huu unamshangaza Ngwese (uk. 45). Hata hivyo, Ngwese

anatumia ufisadi na kubatilisha ushindi huu. Baada ya kuwagawia wananchi matunda, baadhi ya wananchi wanabadili msimamo wao na kumuunga Ngwese mkono (uk. 47-48). Katango kwa ukakamavu anaendelea kupigania mabadiliko ya uongozi. Baada ya Ngwese kutangazwa mshindi, anaendeleza utepetevu na uongozi mbaya. Hata haendi kazini (uk. 51). Inapodhihirika kuwa Katango alisema ukweli kuwa Ngwese analiharibu Pango na kurina asali, kundi la wananchi linamsherehekea Katango (uk. 86). Katango anasogea katikati na kuanza kuongea. Ni wakati huu ndipo askari wanafika na kumtia Ngwese mbaroni kwa tuhuma za ufisadi (uk. 87). Huu unakuwa mwisho wa uongozi wa Ngwese. Katango anaibuka kiongozi wa Pango.

Ushindi wa mwanamke kiongozi katika tamthilia teule unaleta furaha na matumaini makubwa katika jamii. Kupitia *Pango* (2003), Katango anapoibuka mshindi, wananchi wanafuatana huku wakicheza kwa furaha. Mwandishi anatueleza furaha hii anaposema:

> Wote (wananchi) wanashikana mikono na kuimba kwa furaha kubwa. Katango anaendelea kuinuliwa juu. Wanaondoka wakiimba wimbo huo kwa sauti ya juu. Mlio wa ngoma unaendelea mpaka taa zinapofifia kabisa (uk. 88).

Kwa mujibu wa Nadharia ya Udenguzi, maana mbalimbali zinaweza kuibuliwa kwa kuchunguza kwa makini lugha iliyotumiwa katika matini (Mung'atha, 2012). Kwa kuchunguza maneno yafuatayo yaliyotumiwa katika maelezo ya mwandishi: "kuimba kwa furaha, kuinuliwa juu, sauti ya juu na mlio wa ngoma", maana mbili zinajitokeza. Moja ni kuwa Wanapango walikuwa na furaha kubwa kuhusu ushindi wa Katango. Pili ni kuwa walikuwa na matumaini makubwa kwa kiongozi wao Katango.

**4.0 Muhtasari kuhusu Uongozi wa Mwanamke katika Tamthilia ya *Kigogo***

Kupitia tamthilia ya *Kigogo* (2016) mwanamke Tunu anaongoza maandamano na kuwahutubia wananchi na wanahabari (uk. 32). Tendo la Tunu kujitokeza kuongoza maandamano ili kuleta mabadiliko ni la kijasiri kwani wanawake hawakuwahi kuongoza jimbo la Sagamoyo. Awali jimbo hili lilikuwa limeongozwa na wanaume kama Ngao na Marara (uk. 4), ndipo maana Kenga anasema kwamba Sagamoyo haijawahi kuwa na wanawake viongozi (uk. 10). Jamii ya Sagamoyo wakati huo haikumruhusu mwanamke kuwa kiongozi si kwa sababu hakuwa na uwezo wa kuongoza ila utamaduni ulisisitiza kuwa mwanamke alikuwa kiumbe duni asiyefaa kuongoza.Tunu anatetea kufunguliwa kwa soko la Chapakazi ambalo lilifungwa na Majoka ili ajenge hoteli ya kifahari katika ardhi hiyo. Aidha, anatetea huduma kuletwa karibu na wananchi na ajira kwa vijana (uk. 54-56). Hata hivyo, anapitia

madhila ya kutamausha. Anasingiziwa kuwa ni mpenzi wa Sudi (uk. 64). Majoka alisababisha kifo cha babake Tunu ambaye alikuwa mfanyakazi katika kiwanda chake (uk. 44). Anapanga njama ya kumuua Tunu (uk. 55). Kenga anapomwambia Majoka kuwa Tunu bado yuko hai, Majoka anashangaa kuwa Tunu amefufuka kutoka kwa wafu (uk. 68). Kutokana na tukio hili la kinyama, Tunu analemazwa miguu hivyo inambidi atumie kiti cha magurudumu. Kenga akimrejelea Tunu anamwambia Majoka: "Hana miguu kwa sasa. Pengine atambae kwa tumbo kama nyoka ..." (uk. 69). Akiwa katika hali hii ya ulemavu, tunatarajia kuwa Tunu ataacha shughuli za kuwahamasisha na kutetea haki za Wanasagamoyo hata kama ni kwa muda. Kinaya ni kuwa Tunu hasitishi harakati zake hata kidogo. Anaamua kwenda kukutana na majangili waliomvamia licha ya mamake kumkataza asiende. Pindi Sudi anapoingia Tunu anamwambia mamake: "Mama, nipeleke bafuni. Tutatoka sasa hivi na Sudi" (uk. 56).

Katika hali yake ya ulemavu, Tunu anafanikiwa kuwahamasisha Wanasagamoyo kukutana kwenye soko la Chapakazi siku ya sherehe za uhuru. Katika mkutano huu, Tunu anahutubu kwa ukakamavu:

> Naomba kwanza kuukosoa uneni wa hapo awali wa viongozi wetu katika vyombo vya habari kwamba siwezi kuzipigania haki za Wanasagamoyo kwa kuwa wamenilemaza. Hali yangu hii ni ya muda tu... (uk. 88-89).

Tunu anapitia changamoto kubwa ikiwamo kutaka kuuawa na hatimaye kuvunjwa mguu. Inabainika katika hotuba hii kwamba Tunu anakataa kukata tamaa katika kutetea haki za Wanasagamoyo baada ya kulemazwa na watu waliotumwa na serikali ya Majoka ili kumwua. Anafaulu kuwashawishi wananchi kukutanika katika lango la soko la Chapakazi ili kutetea haki zao (uk. 88). Wananchi wanasusia mkutano wa Majoka wa kusherehekea miaka sitini ya uhuru. Ni katika mkutano huu ambapo Majoka alinuia kumtambulisha mwanawe Ngao Junior ambaye angechukua nafasi ya kiongozi wa Sagamoyo baada yake (uk. 37). Kifo cha Ngao Junior na kuporomoka kwa uongozi mbaya wa Majoka kunapisha uongozi wa Tunu. Wafuasi wa Majoka kama Kenga aliyekuwa mshauri mkuu wa Majoka na Kingi aliyekuwa mkuu wa polisi wanabadili msimamo wao wa kisiasa na kumuunga mkono Tunu (uk. 91). Awali, Kenga, Chopi, Mwango, Boza na Husda (mkewe Majoka) walikuwa wafuasi wa Majoka. Hawa wakiwa pamoja na Daktari wanamzunguka Majoka na kumtoa mamlakani. Tunu anakwezwa mamlakani (uk. 93). Hatimaye wananchi wanafurahi uongozi wa Majoka unapofikia ukingoni, na Tunu kufanywa kiongozi. Wanamshangilia na kumwimbia Tunu kuonyesha msisimko wao. Sauti ya wananchi inasema: "Hoyee…! Tunu tosha! Tunu …uu! Tunu…uu!" (uk. 89).

Usemi huu unadhihirisha furaha na msisimko wa wananchi kwa kiongozi wao Tunu.

## 5.0 Mitindo ya Lugha Inayojenga Taswira ya Mwanamke Kiongozi

Sehemu hii imejadili mitindo ya lugha inayomsawiri mwanamke kiongozi katika tamthilia za *Pango* na *Kigogo*. Mbinu hizi zimechunguzwa ili kubaini zinavyochangia kujenga taswira ya kiongozi wa jinsi ya kike katika tamthilia teule. Mbinu hizi ni: takriri, maswali ya balagha, methali, jazanda, nahau na misemo, tashbihi na kinaya na kejeli.

### 5.1 Takriri

Takriri ni tamathali ya usemi ambayo kwayo maneno, sauti, wazo au vifungu fulani katika kazi ya fasihi hurudiwa (Senkoro, 1982; Ntarangwi, 2004). Kwa mujibu wa Wamitila (2003) takriri husisitiza na kushadidia ujumbe ili msomaji apate athari ya msisitizo huo. Kwa kurejelea *Pango* (2003), kiongozi Katango anasawiriwa kama kiongozi mkakamavu na mwenye msimamo thabiti kupitia kwa kurudia maneno ‘la’ na ‘siachi’ katika jibu lake kwa mamake aliyemtaka aache kumpinga Ngwese katika uwaniaji wa uongozi wa Pango. Anasema: “La! Mama La! Siachi kabisa siachi!” (uk. 34). Lugha ya mwanamke Katango katika usemi huu inamsawiri kama kiongozi mkakamavu na mwenye msimamo thabiti. Hii inatokana na hali kwamba Katango anayanena maneno haya baada ya kuvamiwa njiani na Mtu I na II. Ngwese anampoka Katango uongozi kifisadi. Baada ya tukio hili, Katango anasema kwa uchungu wakati anabaki peke yake:

> Lakini siachi katu siachi
> Kulistahi pango siachi
> Ndoto yangu na kizazi changu siachi, siachi!!! (uk. 49).

Wamitila (2008) anaeleza kuwa, takriri ni mbinu ambayo hutumiwa kwa ajili ya kusisitiza jambo fulani. Uradidi wa neno ‘siachi’ katika dondoo hili unasisitiza ukakamavu wa Katango wa kuendelea na lengo lake la kutaka kuongoza Pango. Kupitia takriri hii Katango amesawiriwa kama kiongozi mkakamavu. Kwa mfano, Kibwana anasifu ushujaa wa Katango: “Shujaa wetu Katango…Katango…Katango…” (uk. 45). Neno Katango linarudiwa katika usemi huu kusheherekea Katango kama kiongozi shupavu. Hili linamsawiri Katango kama kiongozi anayeheshimiwa. Taswira hii vilevile inasawiriwa wakati kundi zima la Wanapango (si vijana pekee kama ilivyokuwa awali) wanamsifu na kumfurahia kupitia urudiaji wa maneno:

> Aiwa! Aiwa! Aiwa! (uk. 86).

Katango oyee! Katango oyee! Katango oyee! (uk. 86).

Katika tamthilia ya *Kigogo* (2016), upendo wa Tunu kwa jamii yake unadhihirika kutokana na maneno yake kwa Sudi: "Jukumu la kulinda uhai. Kulinda haki. Kulinda uhuru" (uk. 18). Tunu anazungumza maneno haya akimshauri Sudi aliyekuwa karibu kukata tamaa. Anamshauri waendelee kupigania uongozi bora. Kwa kurudia neno 'kulinda' picha ya Tunu kama kiongozi mwenye lengo na maono inabainika. Tunu analenga kulinda uhai, haki na uhuru wa Sagamoyo. Aidha, Tunu anapozungumza na wananchi wa jimbo la Sagamoyo, wanamfurahia kupitia kwa takriri kama ifuatavyo:

…Tunu tosha! Tunu…uu! Tunu…uu! (uk. 89).
Tunu juuuu! Tunu…uuu! Tunu…uuu! (uk. 90).

Uradidi wa neno Tunu unadhihirisha namna wananchi walivyoshawishika kupitia kwa matendo na maneno ya Tunu na kumfuata. Uradidi huu unaonyesha hisia za furaha walizokuwa nazo wananchi kwa kiongozi Tunu na kumsawiri kama kiongozi mshawishi.

## 5.2 Maswali ya Balagha

Maswali ya balagha ni maswali ambayo hutumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ambayo hayahitaji majibu (Wamitila, 2003). Kwa maoni ya Nyamari (2013) jibu la swali la balagha huwa akilini mwa anayeulizwa au anayesoma kazi husika au huwa tayari analijua. Maswali ya balagha huwa na dhima ya kutoa mawazo au hisia za ndani za mhusika au kuweka jambo fulani wazi kwa hadhira (Murungi, 2013; Nyamari, 2013). Aidha, hulenga kusisitiza usemi fulani na kuwasilisha maudhui (Nyuta, 2016).

Katika tamthilia ya *Pango* (2003), Ngwese anamuuliza mkewe swali balagha: "Yule mwalimu alipojitia ujasiri aliona nini?" (uk. 51). Katika Nadharia ya Udenguzi, lugha ni kipengele muhimu cha matini kwani kutokana kwayo maana mbalimbali katika matini huweza kuibuliwa (Miller, 1976). Japo swali hili linaonekana kumdunisha kiongozi Katango, linamsawiri kama mtu msomi na jasiri.

Badala ya Katango kujawa na woga anapokutana na mpinzani wake mkuu wa jinsi ya kiume, Katango kwa ujasiri anamjibu Ngwese kwa balagha: "Je, unadhani ubabe wako utanitisha mimi?" (uk. 10). Balagha hii inamchora Katango kama kiongozi jasiri. Katika jamii ya Pango, mwanamke aliyejaribu kwenda kinyume na mfumo wa kitamaduni uliomdhalilisha mwanamke alisawiriwa na kutazamwa kama mwenye kiburi na muasi. Mtu I na II wanataka kumtumia Katango kimapenzi. Kiongozi Katango anapokataa, Mtu II anamwambia:

> Nini kikupacho kiburi au ni hiyo elimu yako. Ahh…unadhani ndiyo nini? Unadhani tumeona wangapi? (uk. 32).

Kwa mujibu wa Nadharia ya Udenguzi, uchunguzi wa matini humwezesha mhakiki kubaini maana mbalimbali katika matini (Miller, 1976). Inabainika katika usemi huu kuwa Katango amechorwa kama msomi. Kando na hayo usemi huu unamchora Katango kama mtu mwenye kiburi. Mtazamo huu vilevile unabainika wakati babake Katango aitwaye Seki anapomwuliza Katango swali balagha: "Ndio huo usasa wenu umekupa kiburi cha kuinua kichwa na kukigotesha jabalini chini kama mjusi?" (uk. 20). Katika balagha hii Katango amesawiriwa kama mtu jasiri anayejitokeza kumpinga mwanaume Ngwese katika kuwania uongozi wa Pango, ingawa Seki ana mtazamo kuwa Katango ni mwenye kiburi. Babake Katango anamwuliza Katango swali lingine balagha: "Eeh niambie, hiyo elimu ya kizungu ndiyo iliyokupa ujasiri wa kuipuuza mila?" (uk.18). Kupitia swali hili la balagha, mwanamke Katango anachorwa kama msomi na mtu jasiri. Hata hivyo, usomi na ujasiri huu unamfanya babake kumwona kama aliyeasi utamaduni wao.

Aidha, tamthilia ya *Pango* (2003) imemchora mwanamke kama kiumbe duni na dhaifu kupitia maswali ya balagha. Seki anamuuliza Katango maswali yafuatayo:

> Utamaduni gani huo? Umesikia wapi wewe mwanamke ameshika mata na mishale katika jamii hii? (uk. 18).
> Utawezaje kufanya jambo ambalo hawafanyi wanawake? (uk. 19).
> Basi niambie pia si kweli unanuia kumpinga kwenye uongozi wa pango? Sema, huo pia si ukweli? (uk. 19).
> Kwanza nawe kwa nini unajitia ushujaa wa kwenda kinyume na utamaduni wetu? Hujui mkia hauongozi kichwa wewe? (uk. 35).

Kulingana na Nadharia ya Udenguzi, lugha iliyotumiwa katika matini huwezesha mchanganuzi kuibua maana mbalimbali (Bakhtin, 1981). Maswali ya Seki kwa mwanawe Katango yanamsawiri mwanamke Katango kama mtu duni asiyeweza na asiyefaa kuongoza. Hata hivyo kupitia kwa maswali haya picha ya mwanamke kama kiongozi mkakamavu anayekiuka mitazamo na matendo hasi yaliyomdunisha na kuwania uongozi inadhihirika. Katango anatetea haki za wanawake kupitia kwa swali la balagha:

> Mwanamke ana nini, si ni mwanapango pia? Si anaweza kuongoza? (uk. 27).
> Sikusema mimi ndiye nifaaye; lakini ikiwa ni mimi kuna ubaya gani? (uk. 21).

Aidha, anatetea haki za watoto anapomwuliza Ngwese maswali mfululizo:

> Watoto gani? Hata hamnazo huachi? Hivi unadhani watu hatuna macho? …Unadhani haya ni nini, madude ya kukamilisha urembo wa uso? Unadhani hayaoni haya? Unasikia, bwa mkubwa? Hukuwafukuza ndugu zangu waliokuja kutafuta maji wewe? Hukuwawinga kama ndege wewe? (uk. 10).

Katika *Kigogo* (2016) Tunu anawaalika Ngurumo, Boza na Wanasagamoyo wengine waliokuwa kwa Mamapima wakibugia mtindi kukutanika sokoni. Ngurumo anazua madai kuwa hawezi kukosa kuhudhuria sherehe za uhuru zitakazoongozwa na kigogo Majoka ili ahudhurie mkutano wa Tunu. Tunu anamdadisi kuhusu uhalisia na ukweli wa msimamo wake: "Gani muhimu kati ya dhifa na soko? Utakula na kunywa dhifa hiyo milele?" (uk. 59). Haya ni maswali ya balagha ambayo hayahitaji majibu na yanamchora kigogo Tunu kama kiongozi anayesema ukweli kwa uwazi.

Majoka anapomwambia Tunu kuwa ana mpango wa kumwoza kwa Ngao Junior, Tunu anamuuliza maswali ili kusisitiza msimamo wake kwamba yeye ni mwanamke wa thamani na anayejiheshimu. Huku akiwa amekasirika, anamdadisi Majoka: "Yaani umenionaje wewe? Waona mimi ni ganda la muwa la juzi? Wadhani siwezi kusubiri kuolewa na mume nimpendaye siyo?" (uk. 42). Katika usemi huu, mtazamo wa Majoka kuwa mwanamke hata akiwa kiongozi ni kiumbe duni na chombo cha mapenzi cha kuolewa tu wala si kuongoza unabainika. Mtazamo huu unamchora Tunu kama kiongozi ambaye anajiheshimu na kutetea hadhi yake katika jamii. Vilevile, Ngurumo na Asiya wanajaribu kuwashawishi Tunu na Sudi wanywe pombe. Asiya anapowaletea pombe akidai ni ya watu mashuhuri, Tunu habadili msimamo wake wa kutokunywa pombe. Anamkemea Asiya kupitia kwa swali balagha: "Koma! Wajua ni hatia kuuza pombe haramu?" (uk. 61). Usemi huu unabainisha msimamo thabiti wa Tunu. Aidha, unaonesha namna Tunu alivyo msema kweli. Maswali ya balagha yametumiwa kumsawiri mwanamke kama mtetezi wa haki zake, za wanawake wenzake na jamii nzima kwa ujumla.

## 5.3 Methali

Methali ni kauli fupi iliyosheheni maana na ujumbe, iliyo na mizizi katika jamii na inayochukuliwa na jamii kuwa kiwakilishi cha hekima na busara (Murungi, 2013; Mturo, 2011). Kwa kurejelea msingi wa lugha katika Nadharia ya Udenguzi, ni vigumu kuibua maana ndani ya matini bila kuchunguza lugha iliyotumiwa (Ntarangwi, 2004). Njogu na Chimerah wanasema kuwa taswira hutokana na maneno yaliyoteuliwa kwa ufundi katika kazi ya fasihi. Matumizi ya mbinu ya

methali katika tamthilia za Kiswahili yanaibua pia taswira ya kiongozi wa jinsi ya kike.

Katika muktadha wa utamaduni wa Pango, mwanamke hakuruhusiwa kuongoza. Ni katika muktadha huu ambapo Ngwese anatumia methali: *Kelele za chura hazimzuii ndovu kunywa maji* na *Kelele za mlango hazimnyimi mwenye nyumba usingizi* (uk. 13). Kwa kutumia methali hizi mbili, Ngwese anasisitiza kuwa atakuwa kiongozi wa Pango licha ya pingamizi la Katango. Anaziona juhudi za Katango za kuwa kiongozi kama juhudi dhaifu zisizoweza kuzuia ndoto yake ya kuongoza Pango. Mwanamke Katango anachorwa hapa kama kiongozi mkakamavu ambaye anajibidiisha kuongoza licha ya mila na tamaduni katika jamii yake zilizompinga. Ni taswira hii inayobainika wakati Babake Katango anamtisha Katango kwa kutumia methali: *Mnyama mwenye mkia mrefu hauvuki moto; atachomeka* (uk. 22).

Katika *Kigogo* (2016), Majoka anamwambia Tunu: *Yaliyopita si ndwele, tuyape mgongo* (uk. 39). Majoka anatumia methali hii baada ya Tunu kumweleza ukweli kuhusu dhuluma ambazo Majoka alimtendea babake Tunu. Maana inayoibuka hapa ni kuwa Majoka anakubali kuwa alimtendea babake Tunu dhuluma. Taswira ya Tunu inayobainika kupitia methali hii ni kiongozi anayesema ukweli kwa uwazi.

Aidha, Majoka anasema: *Asante ya punda ni mateke* (uk. 44). Majoka anatumia methali hii ili kumsingizia Tunu kuwa mtu asiye na shukrani. Kwa mujibu wa Mwamzandi (2013), Nadharia ya Udenguzi huchunguza matini kwa makini ili kubaini kivuli cha maana ndani ya matini. Kulingana naye, kivuli cha maana ni ile sehemu ya pili ya neno au dhana ambayo huenda isizungumziwe waziwazi na mwandishi. Kwa kuchunguza methali hii tunajiuliza ikiwa Tunu alikuwa mtu asiye na shukrani. Ukweli ni kuwa Tunu alikuwa kiongozi mwenye shukrani. Mathalani, anawashukuru wananchi kwa kumpa fursa kuwahutubia (uk. 88). Kivuli cha maana ni kuwa Tunu amesawiriwa kupitia methali hii kama kiongozi mkakamavu kwani anavumilia singizio kutoka kwa Majoka.

Isitoshe, Tunu ananena na Majoka kupitia methali: *Mla na miwili hana mwisho mwema* (uk. 41). Methali hii ina maana kuwa, mtu mbinafsi hupata hasara baadaye. Methali hii inamsawiri Tunu kama mwenye hekima, hivyo methali hii inatumika kukosoa ubinafsi wa Majoka. Huenda angemkasirisha Majoka iwapo angemwambia moja kwa moja kuwa alikuwa kiongozi mbinafsi.

### 5.4 Jazanda

Kulingana na Njogu na Chimerah (1999) jazanda ni mbinu ambayo hutumiwa kuelezea hali ambapo hadithi inaweza kufasiriwa kwa namna tofauti. Kulingana naye, wahusika na matukio yanayopatikana katika hadithi hiyo huwa na maana

nyingine zaidi ya ile ya kijuujuu. Jazanda ni sawa na kilichositiriwa (Nyuta, 2016). Kwa mujibu wa Nadharia ya Udenguzi, lugha hutekeleza wajibu muhimu katika kuibua maana katika matini husika (Ntarangwi, 2004).

Katika tamthilia ya *Pango* (2003) mbinu ya jazanda inajitokeza katika semi za wahusika mbalimbali ambayo inajenga taswira ya mwanamke kiongozi. Seki, babake Katango, anamwuliza Katango swali la balagha: "Hujui *mkia* hauongozi *kichwa* wewe?" (uk. 35). Seki katika usemi huu anatumia jazanda ya kichwa na mkia. Kwa kurejelea mhimili wa lugha katika Nadharia ya Udenguzi, maneno ndani ya matini husheheni maana (Miller, 1976). Kichwa ni sehemu ya mwili ambayo huongoza mwili mzima na hubeba ubongo, macho, masikio na viungo vingine. Sehemu hii huwa ya juu kwa binadamu na mbele kwa wanyama. Neno kichwa limetumiwa kijazanda kusisitiza kuwa wanaume katika Pango walifaa kuongoza jamii. Mkia kwa upande mwingine ni sehemu ya mwili ambayo hufuata mahali kichwa cha mnyama huongoza. Aghalabu sehemu hii huwa si muhimu sana ikilinganishwa na kichwa. Mathalani, kuna wanyama ambao hata sehemu hii ikiondolewa, maisha yao huendelea. Kwa mfano, mkia ukiondolewa kwa kondoo, maisha yake huendelea na hata hunona zaidi. Binadamu hana mkia. Kwa kumlinganisha mwanamke (Katango) na mkia, Seki ana maana kuwa kulingana na muktadha wa utamaduni wa Pango, mwanamke anafaa daima kuongozwa. Yeye si mtu muhimu sana kwa kuwa kama mkia jamii inaweza kuendelea bila yeye. Jazanda ya mkia katika usemi wa Ngwese inamchora mwanamke kama kiumbe duni na dhaifu ambaye hafai kuongoza jamii na ambaye daima anafaa amnyenyekee na kumfuata mwanamume. Kwa mujibu wa Mugambi (1982), mwanamke katika tamthilia za awali alisawiriwa kama kiumbe dhaifu ambaye hana upeo mkubwa wa kisiasa na ambao alitarajiwa kuchukua maagizo kutoka kwa waume wao bila ukinzani. Wanaudenguzi hushikilia kuwa mhakiki wa matini aweza kuibua maana mbalimbali ndani ya matini. Jazanda hii ya mkia inaweza kumsawiri Katango kama mawanamke dhaifu asiyefaa kuongoza. Hata hivyo, uchunguzi wa kina wa muktadha wa jamii ya Pango, jazanda hii inamchora Katanga kama kiongozi jasiri kwa kuwa Katango anajitokeza kuwania uongozi wa Pango licha ya taasubi ya kiume iliyokuwapo.

Jazanda nyingine katika tamthilia hii inajitokeza Kikubi anaposema: "Eeh, Katango *jiwe la mango*, amchezeaye huvunjwa maungo" (uk. 39). Lugha kama kipengele kimojawapo muhimu cha Nadharia ya Udenguzi husisitiza uelewa wa lugha iliyotumiwa ndani mwa matini ili kufasiri maana (Ntaragwi, 2004). Uelewa wa jazanda jiwe la mango katika usemi huu ni muhimu katika kuelewa maana. Jiwe la mango ni jiwe gumu sana lenye umbo la mviringo. Jiwe hili ni imara na thabiti. Jazanda hii inasisitiza kuwa mwanamke Katango hatetereki. Msimamo thabiti wa Katango unabainika wakati anakataa kusita kuwania uongozi wa Pango na

kupigania maslahi ya Wanapango licha ya changamoto nyingi anazopitia. Mwishowe, Katango anaibuka mshindi baada ya Ngwese kutiwa nguvuni. Jazanda ya jiwe la mango inamsawiri kiongozi Katango kama mwenye msimamo thabiti usiotetereka. Katango anasema kuwa mwanamke ni nguzo (uk. 27). Nguzo ni kipande cha mti au chuma kilichosimamishwa wima ardhini ili kuhimili au kushikilia kitu kingine kama vile paa la nyumba (TUKI, 2014). Nguzo huwa muhimu sana katika kuhakikisha kuwa nyumba ni imara. Pasipo na nguzo hapawezi kuwapo na nyumba. Kwa mujibu wa Nadharia ya Udenguzi, maana hufasiriwa kwa kuchunguza mitazamo iliyopo (Ntarangwi, 2004). Hivyo basi, mtazamo wa Katango ni kuwa mwanamke ni kiumbe muhimu sana katika jamii na bila kuwapo mwanamke hapawezi kuwapo na jamii. Katango anatetea haki ya mwanamke kuongoza kwani anajiona kama mhimili muhimu katika maendeleo ya jamii. Kupitia kwa jazanda hii, Katango anajisawiri kama mtetezi wa jinsi ya kike.

Aidha, Katango anauambia umati wakati wa kampeni za kuwania uongozi wa Pango: "Usisahau ni *kiwavi* anayeishia kuzaa *kipepeo*" (uk. 48). Kwa mujibu wa Derrida (1976), kila neno huwa na maana iliyojengwa ndani mwake na aghalabu huhusiana na neno lingine. Neno Kiwavi katika usemi huu wa Katango lina maana ya mdudu mwenye miguu mingi ambaye aghalabu huwa na manyoya yanayowasha na aliye katika hatua ya pili ya ukuaji wa vipepeo na nondo. Kipepeo ni mdudu mwenye umbo jembamba na mbawa pana zenye rangi mbalimbali na kupendelea kutua kwenye maua (TUKI, 2004). Kwa mujibu wa Mung'atha (2012) Nadharia ya Udenguzi hulenga kufichua maana ndani mwa matini ambayo huwa imefichwa na mwandishi kupitia vipengele vya lugha. Kupitia jazanda ya kiwavi na kipepeo, tunabaini kuwa Katango ni mtetezi wa haki za vijana. Anatetea haki ya vijana ya kuongoza namna afanyavyo kipepeo anapopaa.

Kijazanda, Katango analinganisha vijana na *moyo wa binadamu* na *damu ya uhai* (uk. 42). Moyo ni kiungo muhimu cha uhai wa binadamu. Moyo ukikosa kufanya kazi binadamu hufa. Uhai wa kiumbe yeyote huwa katika damu yake. Mwanadamu akiishiwa damu mwilini hufa. Kwa kutumia jazanda ya moyo na damu, Katango anatetea haki ya vijana ya kutambuliwa kuwa watu muhimu wa kuiongoza jamii kufikia malengo yake. Mbinu hii inamchora mwanamke Katango kama mtetezi wa vijana.

Kundi la vijana katika uwanja wa kampeni linatumia jazanda ya *kikaango* kumwita Katango (uk. 27). Kikaango ni chombo kitumiwacho kukaangia vyakula (TUKI, 2004). Hakuna siku kikaango kitakataa kukaanga chakula. Kundi hili lina mtazamo kuwa Katango ni kikaango cha Ngwese kwa kuwa atakomesha uongozi mbaya wa Ngwese. Taswira ya kiongozi Katango inayojitokeza kutokana na jazanda hii ni kiongozi jasiri na mkakamavu.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kigogo* (2016), Kenga anamshauri Majoka: "Limekuwa *donda ndugu* sasa" (uk. 35). Jazanda ya donda ndugu iliyotumiwa katika dondoo hili inarejelea joto la kisiasa jimboni ambapo Tunu alikuwa amefaulu kuwashawishi na kuwazindua wananchi kupinga uongozi wa Majoka na kutetea haki zao. Jazanda hii ni dhihirisho la ushawishi wa Tunu na inamsawiri Tunu kama kiongozi mshawishi. Aidha, *Kinyago* cha Tunu alichochonga Sudi (uk.10, 93) ni jazanda inayobainisha namna mwanamke alivyokwezwa katika jamii ya Sagamoyo. Jazanda hii inamchora mwanamke Tunu kama kiongozi anayeheshimiwa.

**5.5 Tashbihi**

Tashbihi ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa kulinganisha vitu viwili ambavyo vina sifa tofauti kwa kutumia maneno kama vile: ja, mfano wa, mithili ya, kama na sawasawa (Njogu na Chimerah, 1999; Wamitila, 2003). Mbinu ya tashibihi vilevile inabainika katika tamthilia ya *Pango* (2003). Mwandishi anaeleza hivi:

> ...Wakati huu anaingia Ngwese kutoka upande wa pili. Anatembea haraka haraka lakini anapomwona Katango anatua ghafla kama aliyemwona zimwi... (uk. 8).

Kwa kurejelea msingi wa lugha katika Nadharia ya Udenguzi, uchunguzi wa kina wa maneno yaliyotumiwa ndani ya matini ni jambo muhimu kwa kuwa kupitia kwayo, maana ya ndani ya maneno haya huibuliwa (Derrida, 1973; Miller 1976). Katango anamithilishwa na zimwi. Neno zimwi lina maana ya kiumbe adhaniwaye na kuaminiwa kuwa huishi msituni na ambaye huweza kujibadilisha katika hali mbalimbali na huweza pia kudhuru (Mdee, Njogu na Shafi, 2011). Umithilishaji huu unabainisha na kusisitiza mtazamo aliokuwa nao Ngwese kwa Katango. Ngwese ana mtazamo kuwa Katango ni nuksi. Mtazamo huu unamsawiri mwanamke Katango kama mkosi. Mwamzandi (2013) akieleza dhana ya kivuli cha maana katika misingi ya Nadharia ya Udenguzi, anasema kuwa kivuli cha maana ni ile sehemu ya pili ya dhana au neno ambayo haiwezi kubainika bila uchunguzi wa kina wa matini. Kwa kuchunguza tendo la Katango la kugombea uongozi, kivuli cha maana kinachojitokeza kutokana na maelezo haya ya mwandishi ni kuwa Katango ni kiongozi mkakamavu. Licha ya mtazamo hasi wa Ngwese unaomlinganisha na zimwi, anaendelea kupigania uongozi.

Katango katika mazungumzo yake na Ngwese anatumia tashibihi: *Ni ukweli na unanyonyota ngozini kama upupu* (uk. 14). Katika usemi huu, Katango anamsisitizia Ngwese kuwa babu yake hakufanywa kuwa chifu kwa kuwa alikuwa kibaraka wa wakoloni wala hakuonewa wivu na wazee wa Katango namna alivyodai Ngwese. Ngwese anakasirishwa na ukweli huu mchungu. Katango anamithilisha ukweli huu mchungu na upupu ambao ukianguka kwenye ngozi

huwasha. Taswira ya mwanamke kiongozi ambaye anawakilishwa na Katango ni ya mtu jasiri na msema kweli kwa uwazi hata kama ukweli huu ni mchungu.

Aidha, mbinu ya tashbihi imedhihirika katika tamthilia ya *Kigogo* (2016). Tunu anamkosoa Majoka kwa uwazi: *Na wala si kuwaua watu kama kuku na kuchekacheka…* (uk. 44). Tunu analinganisha mauaji anayoyatekeleza Majoka na mauaji ya kuku. Picha ya Tunu ambaye ni kiwakilishi cha mwanamke kiongozi inayobainika katika usemi huu ni ya mtu jasiri na msema kweli kwa uwazi. Tunu hasiti kumkosoa Majoka kwa mauaji ya Wanasagamoyo anayoyaendeleza.

Vilevile, Boza anatumia mbinu ya tashbihi anapomkemea Sudi: Una mke na bado *mnafwatana kama mtu na kivuli chake*… (uk. 6). Boza anamithilisha namna Sudi anavyomwandama Tunu. Kwa mujibu wa utamaduni wa jimbo la Sagamoyo, mwanamke anapoandamana na mwanaume yeyote basi inaaminika kwamba wanashiriki mapenzi. Kwa kuangazia usemi huu wa Boza na kwa misingi ya mtazamo huu wa kitamaduni, Tunu anasawiriwa kama chombo cha mapenzi. Hata hivyo, kwa kuchunguza usemi huu kwa misingi ya matendo ya Tunu katika tamthilia hii, tunapata kutambua kivuli cha maana kuwa Tunu anamshawishi Sudi hadi Sudi anaambatana naye katika juhudi za kutetetea haki za Wanasagamoyo. Mwamzandi (2013) anaeleza kuwa kivuli cha maana kwa mujibu wa udenguzi ni ile sehemu ya pili ya dhana ambayo huenda isibainishwe iwapo matini haitachunguzwa kwa makini.

Kenga anatumia tashbihi ya nyoka ambaye hutambaa kutokana na ukosefu wa miguu kuelezea hali ya Tunu: Hana miguu kwa sasa pengine *atambae kwa tumbo kama nyoka*! (uk. 69). Usemi huu unaweza kumsawiri Tunu kama kiumbe dhaifu anayetendewa madhila ya kila aina. Hata hivyo kwa kuchunguza zaidi tendo la Tunu la kuendelea kutetea uongozi bora wa jimbo lao licha ya ulemavu, taswira ya Tunu kama kiongozi mkakamavu inachoreka. Kwa mujibu wa wanaudenguzi, matini husheheni maana mbalimbali ambazo huibuliwa kupitia uchunguzi wa kina wa matini (Mishra, 2018).

## 5.6 Nahau na Misemo

Nahau ni msemo uliojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida lakini huwa umesetiri maana tofauti na ile inayokuwa imebebwa na maneno hayo hayo katika matumizi ya kawaida (Senkoro 1982, Wamitila, 2003). Kulingana na Mturo (2011) misemo ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea tungo ambazo hutumia picha, ishara na tamathali kuelezea kitu au wazo kwa ufupi. Senkoro (1982) anasema kwamba misemo ni sawa na nahau kimatumizi ila nahau zenyewe ni misemo ambayo huwa imeshika mizizi zaidi katika jamii na huwa na hadhira pana kuliko misemo. Kimsingi, nahau huundwa kutokana na nomino na kitenzi (Wamitila, 2008).

Katika *Pango* (2003), Katango anamwambia Ngwese: “Watoto gani? *Hata hamnazo huachi*?” (uk. 10). Msemo huu *hata hamnazo huachi* unadhihirisha namna Katango alivyotetea haki za watoto. Usemi huu unabainisha mapuuza ya Ngwese kuhusu nafasi ya Watoto katika jamii.

Aidha, Katango anamwambia Mbabekazi: Hatuwezi *kushikilia* tu *chungu cha zamani* na huku wakati unapita (uk. 27). Msemo wa *kushikilia chungu cha zamani* unamaanisha kujikita katika mtazamo wa kitamaduni. Anachosisitiza Katango kupitia usemi huu ni kuwa kama wanawake hawakufaa kushikilia mtazamo wa kitamaduni uliowadhalilisha wanawake kuhusiana na suala la uongozi; wanafaa kujitokeza na kuwania nyadhifa za uongozi. Msemo huu unamchora Katango kama kiongozi mtetezi wa haki ya wanawake ya kuongoza.

Katika Kigogo (2016), Boza anamwuliza Sudi: Wafikiri *nauza nyonga* kama huyo Tunu wako? (uk. 64). Nahau *uza nyonga* katika swali hili balagha ina maana ya kushiriki katika biashara ya ukahaba. Boza ana mtazamo kuwa Tunu ni mpenziwe Sudi jambo ambalo si kweli. Taswira ya kiongozi Tunu inayojengeka kupitia kwa nahau hii ni ya mwanamke mkakamavu na anayejiheshimu.

Isitoshe, Kenga anamwambia Majoka: *Waliota mizizi* ikakita na *wakamea* hata *pembe* (uk. 35). Nahau mbili zinabainika katika usemi huu: *ota mizizi* na *mea pembe*. Kulingana na Kenga, Tunu pamoja na wafuasi wake wameendelea kupinga uongozi wa Majoka hadi imekuwa vigumu kuwaondoa. Nahau hizi zinamsawiri Tunu kama kiongozi mshawishi na mkakamavu.

**5.7 Kinaya na Kejeli**

Kinaya ni kinyume cha jambo au matarajio. Kejeli ni kusema kwa kukebehi au kumwambia mtu maneno ya kuudhi kwa masihara (Mdee, Njogu na Shafi, 2011). Kulingana na Mishra (2018) Nadharia ya Udenguzi hulenga kubainsha kinaya, utata, ukinzani, unyume na mwachano ndani ya matini kwani kupitia kwa ubainishi huu, maana mbalimbali zilizomo ndani ya matini huibuliwa.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Pango* (2003), Katango anaonyesha ujasiri na ukakamavu wake wakati Mtu I na II wanamvamia njiani akiwa na Kibwana. Huku Mtu wa II akicheka kwa dharau, anamkejeli kiongozi Katango kwa kusema:

> Aahh, unaogopa nini Katango? Iweje anayetaka kuwa mlinzi wa Pango awe mwoga kiasi hiki? Shh…shhh...Pango litaongozwa na mwoga hili? Jama tutapona? (uk. 31).

Katika usemi huu, madai ya Mtu II kuwa Katango ni mwoga ni kinyume cha ukweli kwa kuwa, Katango alipovamiwa na Mtu wa I na II aliwakabili kijeshi na kutaka kuvua vazi alilokuwa amejifunika Mtu I. Kinaya ni kuwa, Mtu II ndiye aliyekuwa

mwoga. Anaposikia Mtu I akipigwa na Kibwana, anatimua mbio na kutoroka kwa uoga. Kinaya hiki kinamchora Katango kama kiongozi jasiri.

Aidha, kwa kurejelea tamthilia ya *Kigogo* (2016) kinaya kinajitokeza wakati Tunu, japo amevunjwa mguu na wahuni, anaondoka nyumbani kwao akiwa katika kiti cha magurudumu na kwenda kukabiliana na wahuni hawa (uk. 56). Awali alimwambia mamake: "Mama, nisimulie kisa haraka ninataka kwenda. Nataka kukutana na majangili" (uk. 55). Tunamtarajia Tunu baada ya kulemazwa atulie nyumbani kwao na hata kuachana na juhudi za kupigania uongozi bora Sagamoyo. Kujitokeza kwa Tunu kwenda kukutana na wahuni pamoja na tendo lake la kuendelea kupigania uongozi bora ni kinyume cha matarajio. Isitoshe, ilikuwa kinyume cha matarajo ya Majoka na washauri wake kuwa Tunu alilemazwa mguu wala hakufariki. Majoka na serikali yake walitarajia kuwa Tunu angekufa kwa kuwa walikuwa wamepanga njama ya kumfisha Tunu (uk. 68). Kinaya hiki kinamsawiri Tunu kama kiongozi jasiri na mkakamavu.

Aidha, Tunu anapowaalika walevi wahudhurie mkutano katika lango la Chapakazi, Ngurumo anamwambia: "Kichwa chako kizuri Tunu? Naona waota ndoto mbaya. Sisi tukose kwenda kwa kigogo wetu kwa dhifa eti tunahudhuria vitu kama hivyo?" (uk. 59). Kwa mujibu wa udenguzi, matini hubeba maana mbalimbali ambazo hubainishwa na mhakiki kupitia usomaji wa kina. Katika muktadha wa kijamii, ukisema kuwa mtu hana kichwa kizuri maana tunayoipata ni kuwa mtu huyo ni mwendawazimu au hana ufahamu (mjinga). Ngurumo anapomwuliza Tunu iwapo kichwa chake ni kizuri, maana mbili zinaibuliwa. Moja ni kuwa Tunu alikuwa mjinga (alikosa ufahamu) na pili ni kuwa Tunu alikuwa mwendawazimu. Kinaya ni kuwa Tunu hakuwa mjinga wala mwendawazimu. Alifahamu haki zake na za Wanasagamoyo. Alikuwa na akili razini ambazo zilimwezesha kupigania uongozi bora. Kinaya ni kuwa Ngurumo ndiye aliyekuwa mjinga (hakuwa na kichwa kizuri) kwa kuwa alimfuata Majoka bila ufahamu wowote. Isitoshe, Ngurumo anamwambia Tunu: "Mbona maringo Tunu!" (uk. 57). Kulingana na Ngurumo, Tunu ana maringo kwa kuwa alikataa kunywa pombe. Tunu kupitia wimbo wa Daudi Kabaka ulioanzishwa na Ngurumo anachorwa kama msichana mrembo ambaye ameelimika sana ila hajaolewa (uk. 65). Msichana huyu ambaye anamithilishwa na Tunu anasemekana kuwa na maringo kwa vijana. Kinaya ni kuwa Tunu hakuwa na maringo kwani alikuja kuwaalika walevi mkutanoni. Ingawa amefikia kiwango cha juu cha elimu, Tunu anahusiana na watu wakiwamo walevi bila kujifaragua. Ukweli ni kuwa Tunu kwa kukataa kunywa pombe, ana msimamo thabiti. Taswira ya mwanamke kiongozi inyodhihirika kupitia kinaya hiki ni ya mwanamke mkakamavu anayevumilia singizio eti ni mwenye majivuno.

Isitoshe, mwandishi anatueleza kuwa Ngurumo anacheka kicheko cha kukera kinachowafanya walevi wengine kukaribia walipo Ngurumo na Boza. Baada

ya kicheko hiki, Ngurumo anamkejeli Tunu: "Tunu wewe ni nani katika Sagamoyo? Babako na babu yako walikuwa nani Sagamoyo?" (uk. 58). Kicheko cha Ngurumo ni cha kumdhihaki Tunu. Kinaya ni kuwa kicheko hiki kinawavutia walevi wengine licha ya mwandishi kutueleza kuwa kilikuwa cha kukera. Kupitia kinaya na kejeli katika muktadha huu, taswira ya mwanamke kama kiongozi jasiri na mkakamavu inabainika. Tunu anajitokeza kwa ujasiri kupigania uongozi bora licha ya kejeli kutoka kwa Ngurumo.

## 6.0 Hitimisho

Lengo la makala hii lilikuwa kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumiwa kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia za *Pango* (2003) na *Kigogo* (2016). Utafiti huu umebaini kuwa mitindo ya lugha imechangia kujenga taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia hizi mbili. Kupitia uchanganuzi wa mitindo mbalimbali ya lugha katika tamthilia teule, picha ya mwanamke kiongozi imebainika.

Makala hii inapendekeza kuwa wahakiki wa baadaye wajitokeze kuchuguza namna uongozi wa mwanamke unavyotofautiana au unavyofanana na wa mwanamume katika fasihi. Katika kuchunguza hili, wajikite katika kubainisha namna lugha ya mwanamke kiongozi na mwanaume kiongozi inavyosababisha utofauti au usawa huu. Aidha, watafiti wa baadaye wachunguze namna lugha ya mwanamke inavyofanikisha au kudidimiza uongozi wake.

## Marejeleo

Derrida, J. (1973). *Speech and Phenomenon.* Evanston*:* North Western University Press.

Hora. E.A. (2014). "Factors that Affect Women Participation in Leadership and Decision Making Position." *Asian Journal of Humanity, Art & Literature*, 1(2): 97-118.

King'ei, K. (2002). "Suala la Uana katika Fasihi ya Kiswahili: Uhakiki wa Utafiti kutoka Kenya." Katika I. Simala (Mh.) *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press. kur. 70-77.

Kohlrieser, G. (2006). *Hostage at the Table: How Leaders can Overcome Conflict, Influence others and Raise Performance*. www.imd.org/.../PFM149_LR_Kohlrieser.pdf. Kur. 36-45. Imesomwa Aprili 5, 2015.

Kombo, K.D. and Tromp, L.A.D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Mapunjo, G.C. (2014). Usawiri wa Mwanamke kama Kiongozi katika Tamthilia ya *Kivuli Kinaisha* na *Nguzo Mama*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks, Graphics & Publishing Company.

Mdee, J.S, Njogu, K na Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Miller, J.H. (1976). "Deconstruction and the Recovery of Transcendence." In G. Douglas Atkins. *Notre Dame English Journal*. 13(1): 52-76.

Mirikau, S.A. (2011). Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Wamitila. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Momanyi, C. (2013). Waliochangia Kukuza Kiswahili miaka 50 ya Uhuru Kenya. www.swahilihub.com/habari/MAKALA/-/1310220/2110676/-/13WS64J/-/index.html. Kur. 15-26. Ilisomwa tarehe 29.9.2015.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugambi, P.J. (1982). Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kenya Zilizochapishwa. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mugenda, O.M. and Mugenda, A.G. (2003). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: African Center for Technology Studies.

Mulila, J.L. (2009). Usawiri Chanya wa Wahusika Wanawake katika Tamthilia za *Zilzala* na *Chamchela*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: The Open University of Tanzania.

Mung'atha, R. (2012). Ufumbuaji wa Mashairi ya Kiswahili: Mfano wa *Malenga wa Mvita* na *Malenga wa Vumba*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Murungi, G.K. (2013). Mtindo Unavyoendelezwa Maudhui katika *Natala*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Murumba, J.B. (2011). Mtindo katika Watu wa Gehenna. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Muthui E.K. (2019). Tathmini ya Maudhui katika Tamthilia Teule za Kiswahili Zinazotahiniwa Shule za Upili nchini Kenya: *Mstahiki Meya* (2009) na *Kigogo* (2016). Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya.

Mwamzandi, I. (2013). "Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia za Fasihi." *Swahili Forum*. 20: 48-66.

Mwangi, D.K. (2005). Uhakiki wa Fani katika Tamthilia za K.W. Wamitila. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwanje, J.I. (2001). *Issues in Social Science Research: Methodology Series Module 1*. Addis Ababa: OSSREA.

Nguta, (2011). Fani na Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia ya *Pango* na *Mama ee*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (2007). *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi.* Rock Island: Augustina College.

Patton, M.Q. (1990). *Qualitative Evaluation and Research Methods* (2nd Ed.). California: Sage.

Suwed. A.A. (2013). Usawiri wa Ujinsia katika Filamu: Uchunguzi wa Matumizi ya Lugha katika Filamu za Steven Kanumba. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Syambo, B na Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Trudgil, P. (1974). *Sociolinguistics*: *An Introduction*. London: Penguin Books.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. New York: Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2003). *Pango*. Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications.

Wamitila, K.W. (2008). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.